

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI YA KISWAHILI
JUNI / JULAI - 2012
SAA 2 ½

MTIHANI WA PAMOJA WA WILAYA YA OLOITOKITOK
Cheti Cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI YA KISWAHILI
JUNI / JULAI - 2012
SAA 2 ½

MAAGIZO KWA MTAHINIWA

- (a) Jibu maswali **manne** pekee katika karatasi za majibu
(b) Swali la **kwanza** ni la **lazima**
(c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani :
Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.
(d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja.**
(e) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

*Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

SEHEMU A: HADITHI FUPI (alama 20)

1. (LAZIMA)

Jadili changamoto zinazoikumba sekta ya elimu katika jamii ukirejelea hadithi zifuatazo:

- (a) Siku ya mganga
- (b) Ndimi za mauti
- (c) Ngome ya nafsi
- (d) Uteuzi wa moyoni.

Jibu swali la 2 au la 3

2. Nimeshakwambia tulale hapa langoni! Tulale umati unaokuja kumtoa mfungwa gerezani utukute hapa. Watu wanatupenda sana kwa kazi ya kumzuia mfungwa gerezani. Kwa hivyo, tuwasubiri waje watupe mafuta.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) (i) Taja mbinu iliyotumika kwenye dondoo (alama 2)

(ii) Fafanua matumizi ya mbinu hii kwenye dondoo. (alama 6)

(c) Ni maovu gani yaliyotekelezwa na wahusika walioko katika dondoo hii (alama 8)

au

3. Jadili huku ukitoa mifano mwafaka matumizi ya mbinu ya uzungumzi nafsia kwenye tamthilia ya Kifo Kisimani. (alama 20)

SEHEMU C: RIWAYA - UTENGANO S.A MOHAMMED.

Jibu swali la 4 au la 5

4. Watu wameshachoka kudanganywa na wanafiki kama nyinyi.’

- (a) Fafanua muktadha wa maneno haya. (alama 4)
- (b) Eleza sifa za msemaji wa maneno haya. (alama 4)
- (c) Wakati wa kisa hiki, msemaji na msemewa wanasababisha aina fulani ya Utengano’. Taja utengano huu na ueleze sababu zake. (alama 4)
- (d) Thibitisha madai kwamba uhuru wa wahusika fulani katika riwaya hii haujatimia. (alama 8)

au

5. Huku ukirejelea wahusika wowote wawili, fafanua mabadiliko kumi yaliyowapata kila mmoja wao. (alama 20)

6. **SEHEMU D: Fasihi Simulizi**

(a) Tambua tamathali zilizotumika katika methali zifuatazo:

(i) Ujana ni moshi ukienda haurudi

(ii) Kupotea njiandiko kujua njia

(iii) Bandu bandu humaliza gogo

(iv) Usipoziba ufa, utajenga ukuta.

(v) Chururu so ndo ndo ndo. (alama 5)

(b) Nyimbo zina umuhimu gani katika jamii? (alama 5)

(c) Eleza aina zifuatazo za ngano:

(i) Khurafa

(ii) Mighani

(iii) Hekaya

(iv) Ngano za mtanziko

(v) Ngano za usuli. (alama 5)

(d) Eleza sifa za ngomezi. (alama 5)

SEHEMU E: Ushairi.

7. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata;

SHAIRI A: HOFU YA BIN – ADAMU

1. Hofu zao wanyonge, ni nguvu za matajiri
Ambazo zinawaponda, wanapotaka usawa.
2. Hofu za watawala, ni kupoteza uhuru,
Wa kutawala kwa mbavu, pamoja na utukufu
3. Hofu za mwanamke, mwanamke wa sasa,
Ni kutumiwa ja rungu, daima kuwekwa nyuma.
4. Hofu za mcha – Mungu, ni maisha ya baadaye,
Maana hana hakika, ndio aogopa kifo.
5. Hofu zao wasomi, ni kwamba wako baidi,
Na wale wateteao, ambao ni sawa nao.

SHAIRI B: AMANI

1. Uhuru pia amani
Usifikirie ni zawadi
Ambayo inapeanwa
Pasipo mikwaruzano
2. Kama wataka hakiyo
Sharutu uwe tayari
Kupoteza roho yako
Pamoja na ya mwingine
3. Uhuru ja ini la fani
Ambalo kulifikia
Sharti uwe jasiri
Jasiri aso kifani

Maswali

- (a) Linganisha bahari za shairi A na B. (alama 4)
- (b) Eleza umbo la kila shairi. (alama 3)
- (c) Andika ubeti wa pili wa shairi B kati lugha nadhari (alama 4)
- (d) Taja na utoe mifano ya mbinu mbili za uandishi zilizotumika katika mashairi yote mawili. (alama 4)
- (e) Taja na utoe mfano wa uhuru wa mtunzi uliotumika katika mashairi yote mawili. (alama 2)

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika mashairi.

(alama 3)

(i) Ja

(ii) Sharuti

(iii) Utukufu